

# Aflasafe KE01™

## Aflatoksini inaua!

Aflasafe hukinga mahindi yako  
dhidi ya athari za aflatoksini



L Kaptoge

H Mwangi/IIITA

**attc**  
**aflasafe**

Aflasafe ni bidhaa ya ki asili ambayo haina madhara kwa mazingira na kwa mkulima – hauhitaji kuvua mavazi ya kujikanga. Hapa, Aiddah Mutua anasambaza Aflasafe katika shamba lake la mahindi, iliyoko Kathiani, Kaunti ya Machakos, Mashariki mwa Kenya, mwezi Desemba mwaka wa 2013. Mashariki mwa Kenya ni eneo ambapo adhari za aflatoksini imekidhiri. Aiddah ni mshirika wa muda mrefu, kama mmoja wa wakulima watangulizi 24 ambao walishiriki kuonyesha kazi ya Aflasafe KE01.

# Aflasafe ni nini, inaundwa vipi na hufanya kazi vipi?

Aflasafe ni bidhaa ambayao ni asili asilimia inayotumiwa kudhibiti sumu ya *Aspergillus flavus* (*A. flavus*) katika mimeya ya vyakula ikiwemo mahindi. Aflasafe hutengenezwa na mtama uliopikwa (asilimia 99 ya bidhaa) ili kuizua isiote, pamoja na aina nne za vijichembe (*A. flavus*) ambazo hazitou sumu; na asili yake ni nchini Kenya. Kisha bidhaa hutumbukizwa kwenye rangi ya samawati ili kuitofautisha na mtama unaofaa kuliwa.

Baada ya kusambazwa na kuwekwa wazi kwenye unyevu wa kutosha, vijichembe nya spora huota na ile rangi ya samawati sasa hufunika na spora za rangi ya kijani. Spora hizi zinapo ota kwanza zitaonekana kama manyoya meupe na kisha kugeuka na kuwa kijani. Spora za rangi ya kijani mwishowe husambaa kwenye mimea, kwa kusambazwa na upepo pamoja na wadudu sawia na namna spora zinazotoa aflatoksinii husambaa.

Aflasafe inaweza kutumiwa kwenye mimea mseto zilizoko kwenye shamba moja. Haitakuwa na madhara yoyote kwenye hizo mimea kwa sababu ni bidhaa asili inayotengenezwa kutokana na dondoo zinazotoka kwenye mimea na udongo wa nchi; pia upanzi wa mimea mseto katika shamba moja hakutaadhiri makali ya Aflasafe.



L. Kaptope

Aflasafe KE01 imetengenezwa nchini Kenya kutokana na jaribio *iliilofanywa* kwenye kiwanda cha Katumani Aflasafe. Rangi ya kijani iliyochapishwa hapo chini ya pakiti inathibitisha kuwa Aflasafe ina viwango nya usalama vya hali ya juu zaidi zilizoratibiwa na Shirika la Afya Duniani. Utengenezaji na usambazaji utafanikishwa na Kenya Agricultural and Livestock Research Organization ambaa ni wadau wetu; na barani Afrika, wadau wengine ni Idara ya Kilimo ya Marekani - almaarufu Agricultural Research Service.

## Maelezo kuhusu matumizi ya Aflasafe

1. Kabla ya kusambaza Aflasafe, shamba linafaa kutayarishwa vizuri ikiwemo kupaliliwa, kuweka mbolea pamoja na kuzingatia mbinu zote za kilimo zilizopendekezwa na wataalamu.
2. Sambaza Aflasafe kwa mkono kiwango cha kilo 10 kwa kila hekta (kilo 4 kwa kila ekari) wiki 2–3 kabla ya mimea kuota maua. Ni bora zaidi, kusambaza Aflasafe baada ya mvua, au mvua inapotabiriwa au wakati ardhii ina unyevu.
3. Hakikisha kuwa Aflasafe inabakia juu ya udongo, ili spora ziweze kunawiri. Kwa hivyo, **USIFANYE SHUGHULI YOYOTE AMBAYO ITACHANGIA AFLASAFE KUFUNIKWA MCHANGANI** baada ya kusambazwa. Shughuli kama hizo zinafaa kufanya mapema kama ilivyoelezwa hapo awali.
4. Baada ya takriban siku 5 hadi 10 baada ya kusambaza Aflasafe, tembelea shamba lako ili kukagua rangi ya Aflasafe iliyosambazwa. Kunafaa kuwepo na uotaji wa spora za rangi ya kijani kwenye baadhi au kwenye mbegu zote za Aflasafe zilizosambazwa; hii utafanikishwa iwapo kuna unyevu wa kutosha kwenye udongo. Ikiwa Aflasafe haijageuka toka samawati hadi kijani, subiri siku 3 hadi 5 kisha urudi kukagua shamba tena.
5. Ili kuhakikisha utenda kazi timiliwa wa Aflasafe, hakikisha umefuata mbinu mwafaka za kilimo na uhifadhi wa mavuno, na pia masharti ya matumizi yaliyochapishwa kwenye pakiti.